



TBL PlcTM



**TANZANIA
BREWRIES
LIMITED**

Taarifa ya Mkutano Mkuu wa 47 wa Wanahisa

TAARIFA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa 47 wa Wanahisa wa Tanzania Breweries Public Limited Company utafanyika tarehe 19 Agosti 2020 kuanzia saa nne asubuhu kwa njia ya mtandao.

Ajenda ya Mkutano ni:

1. **Taarifa ya Mkutano Mkuu**
Taarifa ya Mkutano itasomwa
2. **Kupitia na Kuidhinisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu Uliopita**
Kupitia na kuidhinisha kumbukuimbu za Mkutano Mkuu wa 46 wa wanahisa.
3. **Yatokanayo na Mkutano Mkuu Uliopita**
4. **Kupokea Taarifa ya Fedha na Taarifa ya Wakurugenzi**
Kupitia na kupokea taarifa ya hesabu kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2019
5. **Kuridhia Gawio Lililolipwa la mwaka uliomalizika(?) Tarehe 31 Desemba 2019**
6. **Kuteua Wakaguzi wa nje wa Hesabu**
Kuidhinisha uteuzi wa kampuni ya PricewaterhouseCoopers kuwawakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni kwa kipindi kitakacho koma tarehe 31 Desemba 2020 (The English version says 2020)
7. **Mengineyo**
Mwanahisa mwenye udhuru, anaweza kumteua mwakilishi wake kwa kujaza fomu za uwakilishi (Proxy Form), mwakilishi ataweza kuongea, kuuliza swali na kupiga kura kwa niaba ya Mwanahisa. Aidha, mwakilishi huyo si lazima awe mwanahisa.

Fomu za uwakilishi zitumwe kwa Katibu wa Kampuni kwa barua pepe tblcorporate.communications@ab-inbev.com.

Mwanahisa anayetaka kushiriki katika mkutano huu anapaswa kujisajili na kuambatanisha cheti chake cha hisa au risiti ya CDS na nakala ya kitambulisho kwenye barua pepe hii : tblcorporate.communications@ab-inbev.com.

IMETOLEWA NA BODI YA WAKURUGENZI

Angalizo:

- i. Mwanahisa mwenye mengineyo atume taarifa yake ya mengineyo angalau siku saba kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu

Nyaraka;

Ripoti ya Mwaka, Fomu za Uwakilishi, Kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita na yatokanayo na mkutano mkuu uliopita zinapatikana kwa kubofya; https://anheuserbusch-inbev-my.sharepoint.com/:f/g/personal/abigail_gcn_ab-inbev_com/Er5IUC2ThzNCg8cF7xIQymEBIfmWfV0_mcvF3XIL_3am2A?e=PZBz1u

Kwa ufafanuzi zaidi, tafadhali tuma barua pepe kwa tblcorporate.communications@ab-inbev.com

HUDUMA ZA HISA NA MAULIZO

Huduma zote zinazohusiana na usajili na hisa kwa sasa zinafanywa na Kampuni ya CSD & Registry Company Limited (CSDR). Mwanahisa anayehitaji kubadili taarifa zake, kwa mfano: akaunti, anwani au kutoa taarifa kwamba hajalipwa gawio, anaombwa awasiliane moja kwa moja na CSDR kwa anwani ifuatayo:

Msajili wa Hisa;

CSD & Registry Company Limited;
Kambarage House, Ghorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni S.L.P 70081,
Dar es Salaam, Simu: 0746 160516 / 0677 070414,
Barua Pepe: registrar@csdr.co.tz